KONGAMANO: Meneja Mwandamizi Biashara ya Kilimo wa Benki ya NMB, Carol Nyangaro, akifafanua jambo kuhusu huduma zinazotolewa na benki hiyo wakati wa kongamano la wadau wa sekta ya maziwa nchini, Dar es Salaam jana.

Wadau wa maziwa kuunda ushirika wa wafugaji

Na MWANDISHI WETU
-DAR ES SALAAM

WADAU wa sekta ndogo ya maziwa nchini, wamekubaliana kuunda ushirika wa wafugaji wa maziwa utakaowawezesha kupata ng'ombe bora, mitaji, teknolojia mbalimbali katika kuzalisha, mabanda na lishe bora ili kuongeza maziwa.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika mkutano wa siku mbili wa sekta ndogo ya maziwa, ulioandaliwa kwa kushirikiana na Benki ya NMB, jukwaa la maziwa duniani (GDP), Benki ya Rabo na taasisi ya ILRI uliokuwa na lengo la kuboresha sekta ya maziwa nchini.

Mojawapo ya changamoto kubwa ambayo sekta ya maziwa nchini inakabiliana nayo ni uzalishaji mdogo wa maziwa ambapo kwa siku ni lita 150,000 tu huzalishwa.

Katika hizo zinazoingia viwandani kusindikwa ni lita 56, viwanda vina uwezo wa kuzalisha lita 750,00 kwa siku kwa mwaka lita bilioni 2.4 huzalishwa, lakini ni milioni 56 tu ndio zinasindikwa. Ngombe wa maziwa wapo milioni 1.1.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano huo, Kaimu Msajili wa Bodi ya maziwa nchini (TDB), Dk. Sophia Mlote, alisema wamekubaliana kuunda vikundi vya wafugaji katika mikoa ya Tanzania ili kulisha kiwanda cha Tanga Fresh.

Kiwanda cha Tanga Fresh kina uwezo wa kuzalisha lita 120,000 kwa siku, lakini kwa sasa kinazalisha lita 46,000 tu kwa siku.

Naye Kaimu Msajili wa bodi ya maziwa, alisema pia wamekubaliana kuunda ushirika wa wafugaji waliopo Nyanda za Juu Kusini, ili waweze kulisha viwanda vya Asas mkoani Iringa na kile cha Ndolifa kilichopo Njombe.

Katika ukanda wa Pwani pia mkutano huo wa wadau muhimu wa sekta ndogo ya maziwa wamekubaliana kuunda na ushirika wa wafugaji watakaowezeshwa ili kuwa na maziwa bora na mengi yatakayolisha kiwanda cha Dar Fresh cha jijini Dar es Salaam.

Aidha, Kaimu Msajili alisema Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) pamoja na Benki ya NMB, ndio wadau na washirika wakuu katika juhudi hizo za Serikali za kukuza sekta ndogo ya maziwa.

Meneja Mwandamizi Idara ya Kilimo kutoka Benki ya NMB, Carol Nyangaro, alisema benki tayari imeshakopesha kiasi cha shilingi bilioni 30 kuanzia mwaka 2017, 2018, 2019 kwa wakulima wadogo, wakati, wakubwa na viwanda.

Nyangaro aliwahimiza wakulima, wafugaji na wanaofanya biashara ya maziwa na nyama kujitokeza ili kupata mikopo kutoka katika benki hiyo ambayo imetenga kiasi cha shilingi bilioni 500 kwa ajili yao.

Mkutano huo uliandaliwa kwa kushirikiana kati ya Benki ya NMB, Global Dairy Platform (GDP), Shirika la ILRI na Benki ya Rabo.

Naye Mwakilishi wa Rabo Partnership, mmoja wa waandaaji wa mkutano huo, Frank Nagel, alisema katika mkutano huo mahususi wa kuboresha sekta ndogo ya maziwa, wadau mbalimbali walipata fursa ya kuelezea changamoto na fursa zilizopo katika sekta.

Kanyasu atoa uhakika kwa wamiliki viwanda vya misitu

Na LUSUNGU HELELA
-WMU

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewahakikishia wamiliki wa viwanda vya misitu nchini kuwa atashughulikia ombi lao la kutaka kuongezewa muda wa mikataba yao kutoka miaka miwili hadi mitano ya kupewa mgao wa vitalu vya miti

Pia ameahidi kuyafanyia kazi malalamiko mbalimbali yaliyowasilishwa ofisini kwake na wamiliki hao yakiwemo ya gharama za tozo ya ushuru wa mazao ya misitu (Cess), inayotozwa na Halmashauri za Wilaya ya Mufindi ambayo licha ya Serikali kutoa maagizo ya kuzuia tozo hiyo bado wadau hao wanaendelea kutozwa.

Hayo aliyasema juzi alipokuwa akizungumza na Rais wa Shirikisho la Viwanda vya Misitu Tanzania (Shivimita) na wanachama wa Shirikisho hilo waliomtembelea ofisini kwake jijini Dodoma.

Katika mazungumzo hayo, Rais wa Shivimita, Ben Sulus, alimwomba Naibu Waziri aangalie namna ya kuwasaidia wadau hao waongezewe muda wa mikataba kutoka miaka miwili hadi mitano ya kupewa mgao wa vitalu vya misitu ili waweze kupata mikopo kutoka kwenye Taasisi za kifedha kwa ajili ya kuendeshea viwanda vyao.

Rais huyo alisema kuwa taasisi za kifedha zimekuwa zikiwanyima mikopo kwa kuhofia fedha zao kupotea kutokana na wadau hao kutokuwa na uhakika wa kuongezewa mikataba mara baada ya mikataba yao ya kuvuna magogo ya miaka miwili waliyopewa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Alisema endapo watapewa mikataba ya miaka mitano watakuwa na uhakika wa kuweza kuendeleza viwanda vyao kwa vile taasisi hizo zitaweza kuwapa mikopo watakayoomba na zitakuwa na uhakika wa kurudishiwa fedha hizo.

Maofisa hao wa Benki ya Dunia wametembelea miradi hiyo wakiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Sulemani Jafo.

Akifafanua zaidi kuhusu utekelezaji wa miradi ya DMDP, Chaurembo, alisema katika kufanikisha miradi hiyo wao Temeke waliamua kukopa fedha Benki ya CRDB Sh bilioni 20 ambazo zilitumika kulipa fidia wananchi katika baadhi ya maeneo ili kupisha mradi huo.

Alimweleza Waziri Jafo kuwa pamoja na kukopa fedha hizo, wameendelea kulipa deni bila tatizo na manispaa ya Temeke iko salama kwani utekelezaji wa miradi ya maendeleo unakwenda vizuri.

"Pamoja na kukopa fedha shilingi bilioni 20 kutoka Benki ya CRDB, tunalipa deni bila tatizo. Pia tunaendelea na kutekeleza miradi mbalimbali ndani ya manispaa yetu, hivyo Temeke tuko salama sana," alisema Chaurembo.

Alisema wanatoa ombi kwa Serikali ili kupata fedha hizo za fidia kama ambavyo imefanyika kwa manispaa ya Kinondoni na Ilala, hivyo ni vema Serikali Kuu ikawapa fedha hizo.

Wakati huo huo ametumia fursa hiyo kutoa ombi kwa Benki ya Dunia iwapo bajeti yao itaruhusu waendelee kuisaidia fedha Manispaa ya Temeke na kufafanua kuwa mradi wa DMDP unatekelezwa katika kata 12 na hivyo bado kuna kata nyingine ambazo nazo zinahitaji kuendelezwa.

Kuhusu namna miradi inavyotekelezwa, Chaurembo, alisema viongozi wa Manispaa ya Temeke wakiwamo madiwani wamekuwa makini kuhakikisha thamani ya fedha inayotolewa kwa ajili ya miradi hiyo inakwenda sambamba na ubora wa mradi.

habari kuhusiana na Kongamano la vijana kimataifa kuhusu Kilimo Biashara (Youth Agro Summit International), litakalofanyika Machi 20 hadi 22, katika Ukumbi wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam.

Alisema Serikali katika kuelekea uchumi wa viwanda, inahitaji kuwekeza nguvu kwa vijana kuingia katika Sekta ya Kilimo na kuacha kuzunguka na bahasha ya kaki ya kuomba ajira sehemu mbalimbali katika mashirika na taasisi nchini.

"Vijana wakiingia katika kilimo suala la kutembea na bahasha kwa ajili ya kutafuta ajira litakuwa historia kwani kijana kuendesha kilimo hakuhitaji watu wa kufanya usaili," alisema Hasunga.

Alisema Serikali imedhamiria kuweka mazingira ya kilimo kwenda kisasa kwa kuhakikisha masoko ndani yanakuwa nafasi na ziada kuuza nje ya nchi.

Aidha, alisema kilimo kimekuwa kikilimwa kwa mazoea na kufanya kilimo kuonekana kigumu lakini Serikali ya Awamu ya Tano inakwenda na kilimo cha kisasa kwa kuhusianisha masoko pamoja na viwanda kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao.

"Nchi yoyote duniani inategemea vijana katika kupata maendeleo hivyo Serikali haitawaacha nyuma vijana katika sekta ya kilimo na biashara," alisema.

Aliwataka vijana kuwa na mwamko wa elimu huku wengine wakiwa wataalamu katika fani mbalimbali jambo ambalo litawafanya kuwa chachu ya kilimo na biashara na kufanya vijana waliokata tamaa kuingia katika sekta hiyo.

Alisema takwimu zinaonyesha asilimia 53 ndio wanatumia jembe la mkono katika kilimo huku asilimia 27 wakitumia wanyama katika kuendesha katika kuendesha kilimo chao wakati takwimu zinaonyesha asilimia 20 wanatumia trekta.

Naye Mwenyekiti wa Kongamano la Vijana Kimataifa Kuhusu Kilimo Biashara, Majabi Emmanuel, alisema wanatarajia kuwa na washiriki 1,000 kutoka sehemu mbalimbali ...